



S.L.P. 3817 KIGALI - TEL/FAX : 86871

**MTIHANI WA TAIFA KWA SHULE ZA SEKONDARI
2001/2002.**

SOMO : KISWAHILI I
MCHEPUO : MKONDO WA LUGHA
MUDA : MASAA MATATU (3)

MAELEKEZO :

1. Karatasi hii ina maswali sita (6)
2. Jibu maswali yote
3. Soma maelezo ya kila swali kabla ya kujibu.
4. Kumbuka kuandika nambari yako ya mtihani.
5. Andika nambari ya kila swali unalolijibu.
6. Tumia wino wa bluu au Mweusi tu.
7. Mwandiko wako usomeke vizuri.

SEHEMU YA I.

UFAHAMU

Panya akirukaruka, na kwenda kila mahala,
Hutawala hanashaka, atakacho akakila,
Na paka anapofika, humaliza zake hila,
Paka anapoondoka, ndipo panya hutawala.

Sijifanye hutambui, uwache tabia hii,
Pupanja haifai, Yambiwalo utii
Ijapo chako wadai, nguvu katu hutumii,
Mwenda pole hajikwai, kijikwaa haumii.

Moja na moja timamu, ongeza tano ni saba,
Baada mwaka kutimu, utaujaza mkoba,
Uwe mtu mahashumu, kwa yako nyingi akiba,
Haba na haba fahamu, kuwa yajaza kibaba.

Wawili walo' wakali, walo na nguvu za haja,
Madume wa kwelikweli, shujaa wenye vioja,
Hawapatani asili, wala kukaa pamoja,
Jua fahali wawili, hawakai zizi moja.

Jambo unapolijua, ukasifiwa na mji,
Sizidi kujishaua, kama ulovaa taji,
Ama waharibikiwa, Mwishowe ukajihoji,
Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji.

Wosia kitu kikuu, daraja yake ijuu,
Tokea wote wakuu, wazee na wajukuu,
Ukiitaka nafuu, fuata usemi huu,
Asosikia la mkuu, Mwisho huvunjika guu.

Wakati unaposonga, Mola anapoamuru,
Huna moja lakupinga, ila jambo kukudhuru,
Balaa itakuzonga, huwezi kujinusuru,
Ajali haina kinga, likufikalo shukuru.

Kadiri yako fuata, kilicho sawa na wewe,
Usiritafute vita, kutaka kuadhiriwe,
Mwisho utakuja juta, kwa ujingao Mwenyewe,
Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe.

JIBU MASWALI YOTE YAFUATAYO. (Alama 25)

(a) Toa maana fupi kwa kila msamiati kama ulivyojitokeza shairini.

- (i) Hila
- (ii) Pupa
- (iii) Jikwaa
- (iv) Vioja
- (v) Kujishaua
- (vi) Jihoji
- (vii) Kujinusuru
- (viii) Kadri yako
- (ix) Kuadhiriwa
- (x) Wosia

(b) Orodhesha methali zote zilizojitokeze humu shairini.

(c) Ipi dhima kuu hasa ya msanii huyu

(d) Andika vibwagizo/vituo vya ubeti wa 4 na wa 5.

(e) Itaje methali moja inayosadifu kikamilifu dhima kuu ya shairi hili.

(f) Onyesha vina vya ubeti wa kwanza na wa Mwisho.

(g) « Sivizuri kupambana na mtu akuzidie nguvu au uwezo ».

Ni methali ipi yenye kubeba ujumbe wenye maana hiyo.

SEHEMU YA II – SARUFI.

(Alama 30).

2. a) Andika maana mbili kwa kila sentensi hizi.

- (i) Amechukua picha yangu
- (ii) Yeye alinipiga kura.

b) Bainisha kiima na kiarifu katika sentensi hizi.

- (i) Yule askari maarufu aliyetuzwa na Rais wa Jamhuri, amefariki.
- (ii) Mmojawapo anayechezea timu ile ni mjukuu wake.
- (iii) Kuku mweupe kuliko wote ndiye wangu.

c) Onyesha viwakilishi vilivyo katika sentensi zifuatazo.

- (i) Kule kusikoonekana
- (ii) Kipi kimepotea
- (iii) Yeye alifika jana
- (iv) Umeongezeka
- (v) Anasoma.
- (vi) Wangapi wamechelewa leo ?
- (vii) Changu usikichukue
- (viii) Wembamba wengi wamependeza.
- (ix) Ipi imeletwa ?
- (x) Maziwa haya ni yake.

d) Bainisha tungo hizi ni tungo zipi kwa msingi wa muundo.

- (i) Baba ameondoka
- (ii) Msemakweli amefika na anafundisha.
- (iii) Anapolia.

e) Onyesha mofimu ambatano katika tungo hizi.

- (i) Yule kijana ni kichwa maji sana.
- (ii) Askari kanzu hawa, walimtimua yule mwizi mithiliya swala.

f) Jaza nafasi zilizo achwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi kwenye mabano.

- (i) Viti vimeibiwa (Wetu, yetu, chetu, vyetu)
- (ii) Mfuko wa vitabu umechanika (yake, lake, wake, chake).
- (iii) Msumeno hauwezi kupasua ubao huu (wako, chako, vyako, yako).
- (iv) Paka mdogo panya mkubwa (wamemkamata, amemkamata)
- (v) Unywele ulikuwa ndani ya mkate (huu, hizi, zile, zangu).
- (vi) Kichaa ndicho kinachomponza (lake, wake, chake, zake)

g) Ziweke sentensi hizi katika hali ya Uwingi.

- (i) Huu ni mti mrefu
- (ii) Mlango Mwekundu
- (iii) Mkono wangu unechafuka.
- (iv) Mwembe huu ni mfupi
- (v) Ule ni mzinga wa nyuki.

h) Tungo hizi zipo katika hali yakinishi, ziandike katika hari kanushi.

- (i) Ulisoma
- (ii) Alikimbia
- (iii) Walisimama
- (iv) Wanasimama
- (v) Anakimbia.

SEHEMU YA III. FASIHI

(Alama 30)

3. Toa tofauti tano kati ya hadithi fupi (ngano) na Riwaya.

4. Eleza dhana zifuatazo kwa ufupi kama zinavyotumika.

Katika fasihi ya Kiswahili.

- (i) Mtazamo wa kidhanifu.
- (ii) Mtazamo wa kiyakinifu.
- (iii) Uhakiki.

5. Fasihi ni kioo cha jamii. Jadili kwa mifano iliyohai.

SEHEMU YA IV – UTUNGAJI

(Alama 15).

6. Chagua kichwa cha habari katika hivi vifuatavyo na uandike insha ya maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200.

- Elimu ni msingi wa maendeleo.
- « GACACA » suluhu la Amani nchini.
- Naipenda nchi yangu.
- Watoto wa mitaani – «Maibobo ».

BLANK PAGE